JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

SHULE YA SEKONDARI LUPA,
S.L.P 36,
CHUNYA.
21/11/2020

KUMB:NA:LSS/CDC/STR/2020
NAMBA ZA SIMU
Mkuu wa shule; 0768351777
Makamu mkuu wa shule: 0762039537

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi,
.....
.....

YAH: **MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPA HALMASHAULI YA WILAYA YA CHUNYA MKOA WA MBEYA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

UTANGULIZI
1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechanguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya sekondari Lupa ipo umbali wa kilometa 1.5 mashariki mwa mji mdogo wa Lupatingatinga.
Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 saa 1.30 asubuhi hivyo mwanao anatakiwa kufika shuleni siku hiyo bila kukosa.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2.1 (A) WAVULANA
i. Suruali mbili(2),moja rangi ya kijani kibichi,na nyingine dark blue.
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili (2)(siyo skuna wala raba)
iv. T-shirt na bukuta moja rangi bluu isiyo na maandishi kwa ajiri ya michezo na raba
v. Soksi jozi mbili (2)rangi nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa kuvalia suruali.
vii. Masweta mawili (2) moja rangi ya kijani kibichi na nyingine dark bluu

(B) WASICHANA
i. Sketi mbili (2) ndefu moja kijani kibichi na dark blue mshono rinda box
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili (siyo skuna wala raba)
iv. T-shirt na bukta moja rangi ya bluu na raba kwa ajiri ya michezo.
v. Masweta mawili (2) moja rangi ya kijani kibichi na nyingine dark blue
vi. Soksi jozi mbili (2)rangi nyeupe.

Mahitaji mengine kwa wote

.Fail cover
.Dictionary (Kamusi ya kingereza)
.Daftari zisizo pungua 10 (Counter book)
.Kalamu za kutosha
.Mkebe wa hesabu.

VIFAA VYA USAFI.

Aje na;-
Wavulana:-Ndoo ya lita ishirini,jembe,mfagio wa chelewachelewa na panga
Wasichana:-Ndoo ya lita ishirini,jembe,mfagio wa chelewachelewa na kwanja

3.SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na marekebisho ya sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

(a) Heshima kwa viongozi,Walimu,Wazazi,Wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwaujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhulio mazuri darasani, na katika kila shughuri za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni razima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuri ya shule na nyingine utakayopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wate wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kuwa msafi wa mwili wako,mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwepo ndani ya mipaka ya shule na nje ya mipaka ya shule.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakato wote
(i) Kutunza mali za Umma

3.1 NIDHAMU KWA UJUMLA

(i) Unatakiwa kuishi kwa amani,heshima,na upendo, ni lazima uwaheshimu walimu na
(ii) Ni marufuku kupigana,kutukanana,kuanzisha au kushiriki vurugu za aina yeyote. wafanyakazi wasio walimu waliopo hapa shuleni, pia uwaheshimu wanafunzi wenzako.
(iii) Lazima uthamini mali ya umma na kuitunza,Hii ni pamoja na majengo ya shule ambayo ni nguvu ya wananchi,kama utafanya uharibifu wa aina yeyote mzazi/mlezi atalazimika kufidia gharama za mali husika.
(iv) Ni makosa kutoroka shule.
(v) Ukipatikana na kosa la ulevi,wizi,uasherati,kuoa au kuolewa,kupata au kutoa mimba,kusababisha mimba,kudharau bendera ya Taifa utafukuzwa shule moja kwa moja.
(vi) Shule si mahali pa malumbano ya kisiasa,hivyo hairuhusiwi kutumia mazingira shule kwa shughuli za kisiasa
(vii) Nikosa kuvuta/kuhifadhi sigara,bangi na madawa ya kulevya kunywa au kuuza

pombe,malufuku kuingia katika virabu vya pombe,majumba ya starehe au nyumba ya kufikia wageni (Guest House).

(viii) Kugomea adhabu ni kosa kubwa linaloweza kukufukuzisha shule,matatizo yote kama yapo ni lazima yatatuliwe na kutumia taratibu zilizowekwa hapa shule.

(ix) Ni lazima uonyesha nidhamu ya hali ya juu,ni kosa kutumia lugha chafu,kubishana kuzomea, au kuguna unapoongea na walezi wako.

(x) Fujo,kuzomea,kukaa chini wakati walimu au mkubwa yeyote aingiapo darasani ni utovu wa nidhamu,ni marufuku kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wako wa darasa.

(xi) Ni lazima usimame na kutoa salamu kwa mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita karibu yako

(xii) Unatakiwa kutii na kufuata taratibu nzima ya shule na kutimiza kila kazi unayotakiwa kuifanya hii pamoja na kuhudhulia vipindi vyote vya masomo na kazi ya elimu ya kujitegemea.

(xiii) Lazima kueshimu kengele,hii ni pamoja na kuhudhulia na kuwai sehemu yeyote unayotakiwa bila kuchelewa ukichelewa utachukuliwa hatua za kinidhamu.

(xiv) Ni malifuku kuongea na wageni wakati wa vipindi vya darasani vinaendelea utaongea na wageni wako wakati wa mapumziko na kwa ruhusa maalumu.

(xv) Ni malufuku kutembelea au kuingia nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu,chumba cha walimu (staff room), ofisi zingine bila ruhusa maalumu.

(xvi) Lazima uheshimu tarehe ya kufungua shule, endapo utachelewa kufika shuleni hatua za kinidhamu zitachukuriwa dhidi yako.

(xvii) Ni marufuku kuendesha shughuli za dini mbalmbali na vipindi maalumu vya dini vilivyo katika ratiba ya shule,bila kibali kutoka kwa mkuu wa shule.

4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi

(ii) Kutokuhudhulia masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro

(iii) Kugoma na kuamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu/Walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wotewanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozo wa shule.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara

(x) Uasherati,uhusiano wa jinsia moja kuoa au kuolewa.

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchini

(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

(Xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makudi.

5. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

(a) Fomu ya Uchaguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo imejazwa na Mganga mkuu wa hosptali ya serikali.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai imeambatanishwa.

(c) Fomu ya mzazi kukirii kukubariana na sheria,kanuni na taratibu.

Tafadhari soma kwa makini/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

KILASI E.A
0768351777
MKUU WA SHULE

the Headmaster
Secondary School
P. O. Box 36
Chunya

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
SHULE YA SKONDARI LUPA
FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI
(JAZA FOMU HII KWA UANGALIFU)

1. Jina kamili la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....wilaya.....
3. Kabila .....uraia.....dini.....
4. Jina la mzazi.....
   Anwani ya mzazi.....
   Kazi ya mzazi.....namba ya simu.....

(sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao)

1. Jina la mzazi.....
2. Uhusiano kati ya mlezi na mwanfunzi.....
3. Kazi ya mlezi.....namba ya simu.....
4. Anwani ya mlezi.....
   .....
5. Shule ya msingi atokayo mwanafunzi.....
6. Wakati wa likizo mwanafunziatakwenda wapi.....
7. Maelezo ya mwanafunzi.....
8. Ujuzi (stadi)mwingine.....

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

LUPA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 36,
CHUNYA.
21/11/2020

TO MEDICAL OFFICER
.....
.....
.....

PART A

Mr/miss.....

Please examine the above named as to his / her physical and mental fitness for a full time student in this school, the examination should include the following

1. Hemoglobin .....
2. P.V bleeding.....
3. Sight.....
4. Blood pressure.....
5. Urine for sugar and pregnancy test.....
6. Stool for routine examination.....
7. Asthma.....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy.....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis.....
13. Neurosis.....
14. Venereal diseases .....
15. Other serious disease.....

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(to be completed by government medical officer)

1. I have examined the above named pupil and considered that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling.
2. Other comments.....
   Date .....Name and signature.....
   Designation.....

Official

stamp.....

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
FORM YA KUKUBALI

1. Mimi .....mvulana /msichana, nimekubali kuingia kidato cha.....katika shule ya sekondari Lupa kama mwanafunzi wa kutwa tarehe ..... nitafika bila kuchelewa na kusoma kwa bidii.
2. Nitatii sheria za shule sitajihusisha wala kuchochea mgomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo, nidhamu na kazi za kujitemegea
3. Sahihi ya mwanafunzi.....Tarehe.....

Sehemu ya mzazi au mlezi

1. Mimi .....nimekubali mtoto wangu.....
   Asome katika shule ya sekondari Lupa kuanzia tarehe .....
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua .
3. Ninakuhakishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea
4. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Lupa kama mwanafunzi , hivyo mimi wala mwanangu hatutamsumbia mkuu wa shule wala uongozi wa shule kwa vyovyote
5. Anwani yangu ya kudumu ni
   .....,
   .....
   .....
   Saini.....TAREHE.....